*Jiwe la Kujengea la kiroho na. 135*

# U V U V I O

*"Kwa maana andiko huua bali roho huhuisha" (2Kor.3:6)*

*Sikiliza kile nabii wa Mungu alivyosema juu ya hilo:*

Niko tayari kuweka nafsi yangu katika aya yoyote ya Neno (Biblia), kusema kwamba hiyo ni kweli. Naamini ni Neno la Mungu lililovuviwa. Na naamini kwamba kila Neno lililoko (Bibliani) limevuviwa (2Petro 1:20 –21). Na niko tayari kuyatumainisha maisha yangu wakati wowote juu ya Neno la Mungu na Ahadi zake, kwa maana ni kweli.

Na Neno la Mungu linapowekwa kwenye udongo wenye mbolea wa Mwaminio aliyevuviwa (Matayo 13:23), litazaa hasa kile Mungu amesema lingefanya, kwa sababu haliwezi kushindwa. Ni Neno la milele la Mungu. Linapasa kuwaamsha watu, linapaswa kutuleta kwenye jambo fulani pale Neno linapopokelewa (Matendo 2:41) Na huo ndio uvuvio. Na mtu hayuko kwenye hali, nje ya toba; yeye hayuko kwenye hali ya kulipokea Neno mpaka kwanza awe amevuviwa.

Mwangalie Petro; chini pale alisema ………. Walisema, "watu wananena mwana wa Adamu kuwa ni nani? (Matayo 16:13-18) "Wengine hunena u Yohana mbatizaji, wengine wananena u Eliya. Na wengine hunena kuwa u Yeremia nabii. Na wengine hunena unabii yule ajaye".

Lakini Yesu akajibu akawaambia nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?
Ona, wokovu msingi wake sio juu ya mtu fulani anavyowaza au kufikiri. Ni vile wewe unafikiri juu yake. Msingi wa uponyaji wa kiungu msingi wake sio vile asemavyo yeye anayeshutumu, au kanisa linavyosema; msingi wake ni imani yako kamilifu katika Neno la Mungu lililovuviwa, na jinsi ulivyovuviwa kuliamini hilo. Hicho ndicho kinaleta matokeo, ni uvuvio wako na Neno. Inakufanyia nini wewe?

Sasa, huyu mpendwa Biblia aliye mweusi na wa zamani, naiamini hiyo kwa moyo wangu wote. Kama siyo kweli, hivyo iko makosani, tusingekuwa na chochote chakuhusika nayo. Lakini naamini kwamba kila Neno limevuviwa, na kila Neno lake ni Neno la Mungu mwenyewe. Na ninaamini mtazamo sahihi wa kiakili kulihusu hilo, yoyote ya hizi ahadi za Mungu itazifanya zote zitimie.

Na Neno lote la Mungu kila kipengele vimefungwa pamoja kwa usahihi. Vitabu sitini na sita vilivyoandikwa na watu mbalimbali, tofauti ya mamia ya miaka, na hata moja halipingani na lingine, na kila moja ni kamilifu. Hakuna aina yoyote ya maandiko katika ulimwengu iliyoandikwa kama hiyo.

Katika miaka elfu mbili iliyopita, wamekuwa wakijaribu kuirekebisha sala ya Bwana, kuongeza Neno moja kwake au kutoa Neno kutoka hiyo ili kuifanya iwe nzuri zaidi. Huwezi hata kufanya hivyo Oh ni kamilifu. Ni neno la Mungu.

Na ninaamini Biblia ni Neno la Mungu lililovuviwa (2Tim. 3:16-17) Kila Neno limevuviwa. Siamini eti kiasi hiki hakikuvuviwa, na hiki kimevuviwa. Naamini yote yamevuviwa. Iwe yote iko sahihi au yote imekosewa. Na kama yote imechanganywa, basi hatujui tutafanyaje. Lakini ni kila Neno ni kweli. Niko tayari kuyatoa sadaka maisha yangu wakati wowote kwa ajili ya ile HII ASEMA BWANA iliyoko hapo.

Sasa ni yote iwe imevuviwa au hakuna chochote kilichovuviwa. Naamini kila Neno lake limevuviwa, Limeandikwa na Mungu, kama tunaweza tu kuliweka kwa usahihi mahali pake; ambapo linahusika. Na kama tunaliweka mahali pake, Mungu atatenda na kuliendesha na kulithibitisha neno lake.

Sasa usingeweza kuweka punje ya mahindi katika boksi la vumbi la mbao au majivu, na ikue haitafanya hivyo. Inapasa iwe kwenye udongo ulio mzuri kuifanya ikue, ni sawa hiyo?

Sasa kama mtu amevuviwa naye akasoma neno lililovuviwa, uvuvio huu wa pande hizi mbili unaleta majibu. Haijalishi umejifunza vizuri mpaka wewe mwenyewe uwe umevuviwa. Inachukua uvuvio wako pamoja ………. Na neno lililovuviwa tayari.

Tunachohitaji leo ni uvuvio juu yetu, Mungu apite kati yetu na uvuvio mpya na atupulizie sisi nguvu zake, na upendo wake na yeye mwenyewe, kwamba ingetuvuvia na kutuamsha sisi kuelekea neno lake. Nahalafu neno likiletwa katika Roho ile ya uvuvio, hapo sasa utaona miujiza inatokea, na mambo yakifanyika, kwa sababu hayo mawili yamekuja tu pamoja.

Kama asili yetu imebadilishwa kutoka kwenye mambo ya ulimwengu na kuchukua asili ya Roho Mtakatifu, Mungu atachukua msimamo wake na atakaa ndani yetu. Waamini waliovuviwa wakichukua neno lililovuviwa, haya yote mawili yanaleta matokeo. Inalileta neno liwe na uhai. Ule uvuvio ulioko moyoni mwako unalifanya neno liwe hai kwa sababu………………… .

Unaweza ukachukua mbegu ya mhindi na kuiweka juu ya dawati. Haijalishi imesafishwa vizuri namna gani, inaweza hata ikawa karati kumi na nne, haitazalisha tena mahindi. Haijalishi hilo dawati ni hafifu namna gani, haijalishi ni dhahabu nzuri na iliyo halisi kiasi gani ile bado imekaa hapo, au haijalishi iko mbegu halisi ya mahindi yalio hai kiasi gani, mbegu ya mhindi lazima ianguke katika udongo mchafu wenye mbolea nyingi ili kuleta matokeo. Amina Oh nalipenda hilo.

Nilikuwa na zungumza na mtu siyo muda mrefu uliopita. Alikuwa anajadiliana na mimi akisema "Huoni aibu kusema kwamba Mungu aliziumba mbingu na nchi katika siku sita?"

Nikasema, hivyo ndivyo Biblia imesema. Akasema "Vema tunao ushahidi na tunaweza kuthibitisha kwamba dunia ina mamilioni ya miaka"

Nikasema hiyo haihusiani chochote na hilo. Mwanzo1:1 ilisema "hapo mwanzo Mungu aliziumba Mbingu na Nchi. Muda. Unaona? Hiyo tu. Sasa dunia ilikuwa ukiwa tena utupu na giza". Na nikasema ninaamini kila mbegu ilikuwa pale, kutoka kwenye ustaarabu mwingine au kitu fulani, na mara tu maji yalipoondolewa na jua likaiwakia, ikaota miti na kila kitu".

Ni hivyo hivyo hata kwa wanadamu, ni mfano. Ukungu wote unapoondolewa mbali, na ufunuo wa kweli kwa ile mbegu halisi iliyolala pale ikiwa imerutubishwa, na Nuru ya Injili unaigusa kwa kweli ya neno lililothibitishwa, hiyo itaishi, inao uhai ndani yake ……Nje ya hapo haiwezi kuishi. Haina huo uhai ndani yake.

Majina hayo yaliwekwa katika kitabu cha uzima cha Mwanakondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, yatadhihirika kwa hakika ya kitu chochote. Ndiyo maana Yesu Kristo ameketi pale na akisubiri katika huduma yake ya upatanisho hata ile mbegu ya mwisho. Anajua hasa ni mahali gani pa kutenda.

Sasa tunapoteza utukufu wetu, tunapoteza Imani. Sasa kama tukienda mbali na Imani, tunalichukua Kanisa liwe katika hali ya kiakili. Na mara nyingi, imewaziwa hivi miongoni mwa watu, kwamba kwasababu kusanyiko ni kubwa na wanajengo kubwa, mnara mkubwa uliochongoka, na watu wengi waliovalia vizuri, na wanadhifu na pesa nyingi, kwamba wangeweza hiki na kile, mara nyingi tunawazo kuwa hilo linavuvia ……… kwamba Kanisa hili limevuviwa, au mara nyingi tumewaangalia wahuduma tofauti, wanaoenda nje huku na kuwa na makusanyiko makubwa ya watu, na tunafikiri, wakati mwingine, kwamba hizo ni ishara za uvuvio. Lakini hiyo kwa pamoja siyo kweli. Huo ni uvuvio wa kibinadamu.

Lakini uvuvio halisi unakuja kwa kufanya mapenzi ya Mungu, ikiwa ni mtu mmoja au ni kidogo tu. Ikiwa ni Kanisa kubwa au Kanisa dogo, hiyo haijalishi. Ikiwa yeye ni mzungumzaji mzuri au mtu tu ambaye kwa shida sana anajua ABC's zake, haijalishi. Inategemea ujumbe ambao anauleta. Kama umevuviwa na Neno la Mungu au umevuviwa na mawazo ya kiakili ya ufahamu wa uvuvio wa kibinadamu.

Watu wengine wanaweza kuvuviwa kwa sababu ya mzungumzaji mzuri. Hiyo hailifanyi hilo kuwa sahihi. Wakati mwingine, wanavuviwa, kwa sababu huyo mtu amefundishwa, kiasi kwamba angeziweka pointi zake zote. Hiyo haimaanishi kuwa ni ya Mungu. Unaona? Ni kwa kupitia tu Neno la Mungu la milele na milele, lililobarikiwa tunaweza kupokea uvuvio, na hilo linalolewa na Roho Mtakatifu na kwa Imani tunalipokea.

Sasa, tunamuona mtu huyu mkuu, na kumbuka Ayubu hakuwa na Biblia ya kusoma katika siku zake, yeye alienda tu kwa uvuvio. Alikuwa ni nabii ambaye Neno la Mungu linakuja kwake. Yeye ilibidi tu avuviwe, kwa sababu alijua nafasi yake kwamba yeye alikuwa ni Nabii wa Mungu. Sasa jambo moja tu lilipaswa litoke ni kwamba ilibidi uvuvio uje ndani yake. Na hapo sasa alijua atakalosema litatokea, kwa sababu ilikuwa ni kwa uvuvio.

Hivyo ndivyo Kanisa lipaswavyo, kama liko kwenye utaratibu (limewekwa kwenye utaratibu) lina tu …………… Linayo mitambo tayari, linahitaji tu nguvu za kuendeshea. Usiku wa leo kama tutaweka mitambo tayari, kuiweka mioyo yetu tayari, mambo tuwezayo kufanya, kufuata kila neno, kumfuata kwenye ubatizo, kumfuata katika kila utaratibu ambao ametuambia tufanye kuweka mitambo yote tayari na kusimama pale, hapo sasa tuko tayari kwa nguvu za kuendeshea ziachiliwe, na ni Mungu pekee awezaye kufanya hivyo, na hilo inabidi liingie ndani ya moyo wako ile imani isemayo "Nimeponywa sasa". Hapo sasa haifanyi tofauti ni mazingira gani yapo. Umeponywa kwa vyovyote umeponywa kwa vyovyote, kwa sababu ni Imani, kwa imani umeponywa.

Sasa linapofunuliwa kwako, kwamba wewe mwenyewe umepokea ahadi ya Mungu ………. Uvuvio, wewe ukiwa ni Mkristo umekugusa, huhitaji hata mstari wa maombi. Kitu pekee unachohitaji ni moyo, uliofunguliwa wakati mitambo yote imewekwa tayari, na uache uvuvio udondoke ndani, na hapo hakuna chochote kiwezacho kubadilisha mawazo yako, unacho, tofauti ya hapo haitakufanyia jambo lolote zuri.

Sasa, angalia Ayubu alihitaji njia ya uvuvio, alikuwa nayo imefunguliwa, alikuwa na njia ya kuwasiliana na Mungu kwa uvuvio, alikuwa na njia ya kujiondoa njiani na kuliacha Neno la Mungu liingie ndani (Ayubu 38:1-7). Angalia walivyokuja kumuona kutoka mashariki na kutoka magharibi, watu wakimuangalia yeye kwa sababu walijua alichosema Ayubu ni kweli. Walijua huyo mtu alichosema ni kweli kwa sababu alichotabiri, ndicho kilichotokea. Na hivyo watu walitoka mashariki na magharibi.

Sasa, wakati mwingine hiyo mivuto mikubwa ya imani inakuja wakati wa matatizo. Mara nyingi ni matatizo ndiyo hutuendesha kwenye hali hii. Ni matatizo ndiyo yaliyo mwendesha Ayubu kwenye hali hiyo. Kwa nini ulikuwa mwisho wa maisha yake. Watoto wake walikuwa wamekufa; ngamia zake na vitu vyake vilikuwa vimeharibiwa (Ayubu 1). Na hata maisha yake mwenyewe, alikuwa amepigwa na majipu kutoka taji ya kichwa chake mpaka kwenye soli ya miguu yake. Ilikuwa ni matatizo yamejikusanya yenyewe, pale ndipo ambapo uvuvio ulimjia yeye.

Oo wanaume na wanawake, usiku huu wa leo, kama ungeangalia kwa mzunguko uone vile ambavyo tuko karibu na kule kuja kwa Bwana. Umeweka pembeni na kuacha ule ubatizo wa Roho Mtakatifu, pengine umetegemea msisimko wa aina fulani au kitu fulani ulichokifanya ambacho shetani anaweza kuigiza, na huwezi

kupata Roho Mtakatifu halisi ndani yako kuendelea njia yote katika ahadi za Mungu. Yawezekanaje mtu adai ya kuwa ana Roho Mtakatifu naye akatae Neno moja la hii Biblia ya kuwa siyo sahihi? Huwezi kufanya hivyo.

Haijalishi wewe ni wa kidini jinsi gani, ni makanisa mengi kiasi gani, ni makanisa mengi kiasi gani una uanachama, ni vitabu vingi kiasi gani ambavyo jina lako limeandikwa ndani yake, kama yule Roho Mtakatifu halisi hayuko ndani yako, ambaye ni Neno hili linapodhihirishwa, hutaona ujumbe na saa, kwa sababu ni Roho Mtakatifu anayefanya hivyo. Lakini lazima kiwepo kitu kinachowasha hicho, uvuvio unapokujia. Kama ukimwaga maji ardhini, juu ya ardhi, juu ya ardhi, na hakuna mbegu pale ya kunywesha, itawezaje kuzaa chochote? Hakuna kitu cha kuweza kuzaa. Hiyo inamaanisha, kuwa ni wateule tu wa Mungu watakakao ona hilo (1Wathesalonike 1:4-6, Waefeso 1:3-4).

Wateule wa Mungu waliliona hilo wakati wa Noa, wakati wa Musa, wakati wa Yesu, wakati wa mitume, wakati wa Luther, wakati wa Wesley, wakati wa Pentekoste. Kwa sababu hiyo ilikuwa ndiyo mbegu iliyokuwa duniani wakati uvuvio ulipomwagwa. Sasa, wakati uvuvio umemwagwa ili kumkusanya Bibi Arusi pamoja, ni wale tu walio wateule watakakao ona hilo. Yesu alisema "Nakushukuru, baba kwa kuwa umewaficha mambo haya wenye hekima na akili, na ukawafunulia watoto walio tayari kujifunza" (Matayo 11:25_27). Sasa uvuvio inabidi ulete mguso wake.

Sasa uvuvio ulipomgusa hilo lilifanya hivyo. Akawa nalo hilo. Sasa tunaona kuwa, kuna wakati wa matatizo wakati m'binyo unapotokea. Angalia na uzunguke leo, angalia mazingira tunayoishi; je siyo Sodoma na Gomorah ya kisasa?

Na hatuishi katika wakati wa Luther, wakati wa Wesley, au wakati wa Pentekoste, wakati wa Pentekoste ulikuwa ni wakati tu wakurudisha vipawa kanisani, lakini tunaishi wakati wa jioni tunaishi wakati wa kuitwa kwa Bibi Arusi.

Uvuvio, hivyo ndivyo unavyokujia wewe kama umgonjwa. Hivyo ndivyo unavyokujia ukiwa matesoni. Kitu fulani kinafunuliwa kwako, na unaona kwamba kimefunuliwa kwako, unalinena, "Nimeponywa".

Ndipo Mungu anakuambia linalokupasa kufanya. "Inuka juu na uanze kutembea" Amen. Hapo linakuwa limekwisha, unapoweza kulifanya namna hiyo. Hiyo ndiyo njia ambayo Mungu analifanya hilo, hapo unamuona Mungu akijidhihirisha kupitia wewe.

Jambo lile lile katika Marko 11:23 "Kama ukiuambia mlima huu "Ng'oka" na usione shaka moyoni mwako, lakini unaamini ulilolisema linatokea, unaweza kupata kile ulichosema" Lakini huwezi ukasimama pale ukisitasita ndani ya akili na kusema hilo; inabidi uwe umevuviwa kulisema hilo. Amen.

Sasa, unapopokea uvuvio kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya magonjwa yako, ni saa hiyo ambapo uponyaji wako umekuja. Hiyo ni kweli. Unapopokea kutoka mbinguni, kwamba Yesu alikufa kwa dhambi zako na umelikubali hilo, huhitaji maombi kwa ajili yako tena umeikubali tayari, hiyo imekwisha.

Sasa, tunaweza kuhubiri Neno, tunaweza kulielezea Neno. Lakini inabidi ulikubali Neno. Oh halleluyah. Hiyo ndiyo inaliwasha moto ndugu, unapolipokea hilo, huo ufunuo, kitu fulani kinakujia kutoka kwa yale yasiyoonekana ya ulimwengu ule wa ngambo, inakuja ikiviringika chini kupitia njia ya siri mahali fulani mpaka kwenye nafsi yako ambayo inasema "Sasa naliona hilo". Macho yako yanawaka; midomo yake iliyoinama chini, inanyooka na kucheka. Kila msuli ndani ya mwili wako unaonekana ukifurahi. Jambo fulani linaenda kutendeka jambo fulani …………. Huhitaji kuwa katika mstari wa maombi tena. Umelipata hilo.

Lakini pamoja na hayo, jambo moja juu ya Neno la Mungu, hata haliwezi kuonekana limezeeka, kwa sababu ni Mungu. Hata kidogo halielezeki. Kila kizazi sasa karibu inakaribia miaka elfu mbili na mia nane au zaidi, hili neno limesomwa na wanaume, makuhani na kadhalika na bado halizeeki hata kidogo. Nimekuwa nikilisoma mimi mwenyewe kwa miaka karibu thelathini na mitano. Na kila mara ninapolisoma, naona kitu fulani kipya ambacho nilikiruka wakati uliopita. Kwa sababu limevuviwa na Mungu katika maandiko unaona ni sifa za Mungu zinazungumza wazi na zinawekwa katika maandishi.

Unaona, inabidi utambue sasa, marafiki, uko kwenye hali gani. Hiyo ndiyo sababu kanda hii; nimesema ni kwa ajili ya kanisa (waaminio) tu (unaona?), "kwa kanisa tu". Kama umeitwa kutoka gizani na kuingia uzimani, kutoka mautini kuingia uzimani. Kutoka kwenye mazoea ya kumfahamu Kristo kiakili mpaka kupata ujuzi wa kuzaliwa mara ya pili na kuangalia maisha yako; kwamba unaweka pembeni tabia za dunia, na unasimama kwa ajili ya Kristo, bila kujali; sasa hapo jambo fulani limetendeka. Unaona? Kuna kitu ndani yako, kinakusukuma na kuona njaa, kama ilivyokuwa kwa Yakobo, unapigana miereka na Bwana; Unatembea tofauti baada ya hapo kuna kitu cha tofauti ndani yako, umegeuzwa. Sasa imekuwa ………

Kabla haijafanyika, inabidi ivuviwe kwako. Sijali; ninaweza kusimama hapa na kuhubiri mpaka niwe na ……….. Nywele nilizonazo zinyonyoke zote, mpaka mabega yangu yainame chini na nifikie miaka tisini, ninyi msikilize kila siku; mpaka Mungu alihuishe hilo kwako bado utakuwa kwenye hali ile ile.

Siku mbili nimekuwa nikijifunza na kuomba juu ya hili unaona? Nilisema "Bwana nilisema hili kanisani?" Kitu fulani kikasema liseme. Saa ikaribu. Najisikia Yeye ataniondosha mapema sasa, kwa hiyo nataka ninyi mjue hilo.

]

Nukuu za kiingereza:
Mtazamo wa Mungu ni nani (50-0815) Aya E-25
Msikieni Yeye (56-0930) Aya E-14-17
Yesu akafufuka (56-0405) Aya E-34
Ile alama ya mnyama Aya 15
Yesu Kristo Yule Yule (35 – 0116E) Aya E-34
Mhuri wa nne kitabu cha mihuri uk 292
Kwa Imani Musa Aya E-17
Nimesikia bali sasa naona Aya 80-89, 101-106, 123,128
Njia Mungu aliyoiweka ya kuponywa aya 33
Kusikia kutambua na kutenda Neno Aya 154-155

---

Jiwe la kujengea la kiroho no. 106 kutoka Neno la saa hii iliyo kusanywa na
Gerd Rodeward Friendestr. 69.D-75328 Schomberge Germany phone (+49) 7235-7613 Fax -3306

---

Atakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia. Na kazi ya haraka itaizunguka dunia. Zile mbegu zitaingizwa katika magazeti na vitu vya kusomea mpaka kila mbegu ya Mungu iliyoteuliwa kimbele imesikia hilo (Ndg. Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk. 724).

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*